
Ziara ya Mafunzo ya

# Wakulima



Vikundi vya Wakulima wa Wilaya za Kongwa na Dodoma Vijijini

SUA PROJECT

# Ziara ya Mafunzo ya Wakulima

## Vikundi vya Wakulima wa Wilaya ya Kongwa na Dodoma Vijijini

Juni 2004

**Kimeandikwa na**

Dk. J. G. Lyimo-Macha
Prof. R. E. Malimbwi
Bw. E. Kiranga
Bw. P. Kawamala

**Kimehaririwa na**

Kamati ya mradi:
Prof. L. D. B. Kinabo
Prof. A. J. P. Tarimo
Prof. E. K. Batamuzi

**ISBN: 9987 – 9006 – 7 - 4**

**Kimechapishwa na**

Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima Wadogowadogo Tanzania
(TARP II-SUA Project)
Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo
S.L.P. 3151, Chuo Kikuu,
Morogoro, TANZANIA

Simu: +255 23 2600970 au + 255 23 2603511 ext 4251
Barua pepe: tarp2@suanet.ac.tz, Tovuti: http//www.suanet.ac.tz/tarpII

Chapisho Namba TS2-105
© Haki ya Kunakili: TARP II SUA Project 2004

# Yaliyomo

**Vifupisho** ........................................................................vii

**1. Utangulizi** ........................................................................1

**2. Inades –Formation Tanzania** ......................................1

**3. Lengo la ziara** ..................................................................2

*3.1. Mradi wa jinsia* ........................................................................3

*3.2. Mradi wa mafunzo ya uundaji na uongozi wa vikundi vya wakulima* ........................................................................5

*3.4. Benki mazao* ........................................................................12

*3.5. Chama cha ushirika na mikopo vijijini (CAVi ushirika Ltd)* ..........14

*3.6. Hifadhi ya mazingira na matumizi bora ya udongo* ....................17

*3.7. Ujuzi asili* ........................................................................19

**4. Mafunzo mengine** ......................................................22

**5. Hitimisho** ..................................................................23

**6. Tathmini ya ziara ya mafunzo INADES** ..........................24

*6.1. Tathimini ya wakufunzi wa IF walioshiriki* ..............................24

*6.2. Maoni* ........................................................................25

**7. Viambatanisho 26**

*7.1. Washiriki ziara ya kwanza* ..............................................26

*7.2. Washiriki wa ziara ya pili* ..............................................27

*7.3. Ahadi za wakulima ziara ya Kwanza* ....................................28

*7.4. Ahadi za Wakulima Ziara ya Pili* ........................................31

## Dibaji

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula (MAFS), pamoja na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Norway (NLH), kinatekeleza Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima Wadogowadogo Tanzania.

Lengo mojawapo katika mradi huu ni kuimarisha uhusiano kati ya Wakulima, Watafiti na Wataalamu wa ughani. Ili kufikia lengo hili, mradi umepanga utaratibu wa kuwawezesha wakulima kutembeleana ndani ya kanda zao na kati ya kanda na kanda.

Makala hii inawasilisha ripoti ya ziara mbili zilizofanyika mwezi Aprili na Mei 2004. Ziara hizi ziliwashirikisha wakulima na wataalamu wa ughani kutoka Kanda ya Mashariki ikijumuisha wilaya za Tanga, Pwani, Morogoro na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ikiwajumuisha wakulima na wataalamu wa ughani kutoka Iringa, Mbeya na Rukwa ambao walitembelea wakulima wa wilaya ya Dodoma vijijini na Kongwa, Mkoa wa Dodoma. Washiriki wengine walikuwa ni watafiti kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Taasisi za Utafiti wa Kilimo Mikocheni, Dar es salaam na Uyole, Mbeya na wakufunzi watatu toka INADES-Formation, Dodoma. Chapisho hili pia linapatikana katika lugha ya kiingereza.

*Profesa L. D. B. Kinabo*
*Mratibu Mradi, TARP II-SUA*
*Juni 2004*

## Dibaji

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula (MAFS), pamoja na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Norway (NLH), kinatekeleza Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima Wadogowadogo Tanzania.

Lengo mojawapo katika mradi huu ni kuimarisha uhusiano kati ya Wakulima, Watafiti na Wataalamu wa ughani. Ili kufikia lengo hili, mradi umepanga utaratibu wa kuwawezesha wakulima kutembeleana ndani ya kanda zao na kati ya kanda na kanda.

Makala hii inawasilisha ripoti ya ziara mbili zilizofanyika mwezi Aprili na Mei 2004. Ziara hizi ziliwashirikisha wakulima na wataalamu wa ughani kutoka Kanda ya Mashariki ikijumuisha wilaya za Tanga, Pwani, Morogoro na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ikiwajumuisha wakulima na wataalamu wa ughani kutoka Iringa, Mbeya na Rukwa ambao walitembelea wakulima wa wilaya ya Dodoma vijijini na Kongwa, Mkoa wa Dodoma. Washiriki wengine walikuwa ni watafiti kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Taasisi za Utafiti wa Kilimo Mikocheni, Dar es salaam na Uyole, Mbeya na wakufunzi watatu toka INADES-Formation, Dodoma. Chapisho hili pia linapatikana katika lugha ya kiingereza.

*Profesa L. D. B. Kinabo*
*Mratibu Mradi, TARP II-SUA*
*Juni 2004*

## Vifupisho

| | |
|---|---|
| CAVi | Chama cha akiba vijijini - Mkoka |
| HIV/AIDS | Virusi Vinavyosababisha Upungufu wa Kinga Mwilini. |
| INADES | Taasisi ya Mendeleo ya Kiuchumi na Kijamii, Afrika |
| LVIA | Shirika la Kimataifa la Kujitolea la Walei la Italia |
| MAFS | Wizara ya Kilimo na Chakula |
| MVIWATA | Muungano wa Vikundi vya Wakulima Tanzania |
| NLH | Chuo Kikuu cha Kilimo cha Norway |
| SUA | Chuo Kikuu Cha Sokoine Cha Kilimo. |
| TARP II | Mradi wa Taifa wa Utafiti wa Kilimo Awamu ya Pili. |
| TOSCA | Wakala Rasmi Wanaothibitisha Mbegu, Tanzania |
| ZOSEMU | Kikundi cha Uzalishaji Mbegu cha Zoisa |

# 1. Utangulizi

Mafunzo kwa wakulima, waghani na watafiti hufanyika kwa kutumia njia mbalimbali. Mojawapo ya njia hizo ni ya kutembelea sehemu mbalimbali ambazo shughuli husika zinaendelea ili kujionea wenyewe ni kwa jinsi gani shughuli hizo huendeshwa na wahusika. Wakati mwingine baada ya kuona, wanaziara hujaribu wenyewe baadhi ya shughuli ili kujipa uelewa zaidi. Uzoefu katika mradi huu wa Uhakika wa Chakula na Pato la kaya kwa Wakulima Wadogowadogo umeonesha kwamba mafunzo kwa njia hii, husaidia wanaziara kuiga mafunzo hayo na kuyafanyia kazi pindi warejeapo majumbani kwao.

Ziara hizi mbili za mafunzo zilihusisha wakulima na waghani kutoka mikoa ya Tanga, Pwani, Morogoro, Iringa, Mbeya na Rukwa. Washiriki wengine walikuwa ni watafiti kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Taasisi za Utafiti wa Kilimo Mikocheni, DSM na Uyole, Mbeya na wakufunzi watatu kutoka INADES-Formation, Dodoma. Ziara hizi zilifanyika kwa awamu mbili, awamu ya kwanza ilianza tarehe 19-21,04.2004 na ziara ya pili ilianza tarehe 17-19, 05.2004. Wakulima washiriki walitoka vikundi 24 vya wakulima kutoka katika Kanda ya Mashariki na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini chini ya Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa wakulima wadogowadogo na hasa wanawake (TARPII-SUA). ***Kibwagizo cha ziara kilikuwa Jifunze, Chukua, Tumia.***

# 2. INADES –Formation Tanzania

INADES-Formation Tanzania ni shirika lisilo la kiserikali (NGO) na lisilo la kibiashara linaloendesha shughuli zake katika mikoa ya Dodoma, Morogoro, Singida, Mbeya, Rukwa na Iringa. Makao makuu ya shirika hili yapo Dodoma. Shirika hili lipo chini ya mtandao wa kimataifa uitwao INADES-Formation (INADES).

Lengo la INADES ni kufanya kazi ili kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa wakulima (Vijana, wanawake na wanaume).

Mwaka 1995 wakulima wanaofanya kazi na INADES Tan: waliibua changamoto kuu zifuatazo:

(i) Kumudu matumizi bora ya mali asili katika mazingira
(ii) Kutengeneza sera zinazohusu maendeleo yao kuunda chombo halali cha kisheria cha kuwawakil na kutetea haki na matakwa yao ya kimaendeleo
(iii) Kumudu bei, masoko, mienendo na ubadilishanaji mazao yao
(iv) Kumudu utunzaji na usimamizi wa rasilimali zao ka ngazi ya kaya
(v) Kutambuliwa na kuthaminiwa jinsi walivyo

Kutokana na changamoto zilizotajwa hapo juu miradi ifua ilianzishwa

(i) Mradi wa matumizi bora ya ardhi
(ii) Uundaji na usimamizi wa vikundi na mitandao wakulima
(iii) Mradi wa masoko
(iv) Mradi wa jinsia
(v) Mradi wa kuendeleza ujuzi wa asili

## 3. Lengo la ziara

Lengo la ziara lilikuwa ni kuwawezesha wakulima waweze kujifu na kupata uelewa wa kina kuhusu:-

- Jinsia
- Jinsi gani wanaweza kuunda na kuanzisha vikundi
- Uendeshaji wa shughuli za vikundi
- Jinsi ya kuanzisha na kuendesha benki mazao
- Jinsi ya kuendesha vyama vya ushirika na mikopo
- Hifadhi ya nafaka na mimea shambani kwa kutumia asili
- Matumizi bora ya ardhi

Ni lengo la ziara pia kuwa wakulima hawa wajifunze nadharia na kwa vitendo kutoka kwa wakulima wenzao. Katika ziara hizi mbili waliweza kutembelea miradi iliyoorodheshwa hapo juu.

## 3.1. Mradi wa jinsia

Mradi huu ulitokana na changamoto iliyotolewa na wakulima akina mama. Mchakato wa akina mama uliibua matatizo makubwa yanayo wakabili nayo ni kama yafuatayo:

- Mzigo mkubwa wa kazi
- Afya za watoto
- Kipato kidogo kwa akina mama
- Kuzuia maambukizo ya ukimwi (HIV/AIDS)
- Kutokomeza mila potofu kama vile ukeketaji, kuoa wake wengi na uzazi usio wa mpango
- Uwezo mdogo wa kuzalisha

Washiriki wa ziara walielezwa kuwa utatuzi wa matatizo haya ulifanyika kwa kubuni miradi midogo midogo mbalimbali kama ifuatayo:

### 3.1.1. Mradi wa majiko banifu

Kutokana na sababu kwamba akina mama walikuwa wakitumia muda mwingi sana kwenda porini kutafuta kuni za kupikia ilionekana kuwa ili kumaliza tatizo hili ni lazima kuanzisha mradi wa majiko banifu. Mradi huu umesaidia kupunguza matumizi ya kuni kwa asilimia 75% maana ni kuni kidogo sana hutumika kupikia chakula, mboga na kuchemsha maji ya kunywa. Jiko moja huinjikwa vyungu viwili au vitatu kwa wakati mmoja. Mzigo wa kuni uliokuwa ukitumika kwa juma moja sasa unatumika kwa majuma matatu au hata mwezi. Licha ya kupungua kwa muda wa kutafuta kuni jiko banifu limesaidia sana kuboresha afya za wanawake na watoto kwani jiko hili hutoa moshi nje hivyo akina mama na watoto hawaathiriki na moshi wakati wa kupika. Itakumbukwa kwamba

katika mikoa ya Mwanza na Shinyanga kuna matukio mengi na wanawake vikongwe kuuawa wakituhumiwa uchawi kwa ajili ya kuwa na macho mekundu, hali ambayo husababishwa na moshi unaotakana na matumizi ya kinyesi cha n'gombe au kuni wanazotumia kupikia.

### 3.1.2. Mradi wa lishe kwa watoto na akina mama wajawazito

Chanzo cha afya mbaya kwa watoto ilikuwa ni elimu ndogo kwa kinamama na kutojua jinsi gani ya kutayarisha chakula bora kwa watoto wao. Baada ya kuanzisha **mradi wa lishe kwa watoto na akina mama wajawazito** wakina mama walio wengi walielewa umuhimu wa lishe bora kwa watoto na akina mama wajawazito na hivi kupunguza sana tatizo la afya mbaya kwa watoto na limekuwa linapungua siku hadi siku.

### 3.1.3. Mradi wa kuboresha kipato

Mradi huu ulitokana na tatizo lililojitokeza la kuwa na kipato kidogo kisichotosheleza mahitaji muhimu katika kaya. Tatizo hili limeanza kupungua baada ya wanawake kufundishwa na kuanza miradi midogo midogo kama vile ya upishi wa vyakula (mama lishe), ufugaji wa nyuki na ufugaji wa samaki. Vile vile wamefundishwa jinsi ya kuanzisha shughuli nyingine mbali mbali za kiuchumi.

### 3.1.4. Mradi wa kuzuia maambukizi ya Ukimwi (HIV/AIDS)

Wanawake na wanaume wa eneo lililotembelewa wamekuwa wakielimishwa vyanzo vya maambukizi ya ukimwi, jinsi unavyoambukizwa na dalili za ugonjwa wenyewe. Ukimwi umekuwa ukienea sana vijijini kupitia mila kama vile kuwarithi wajane, kuoa wanawake wengi na vile vile kutumia kisu kimoja kukeketa au

kutahiri zaidi ya mtu mmoja. Licha ya mafunzo hayo wakulima wameelezwa athari za kiuchumi baada ya kuoa wake wengi na kuzaa watoto wengi. Watoto wengi hukimbilia mitaani, hukosa elimu na hata hukosa mapenzi kwa wazazi wao kwa sababu hawawezi kuwatunza na kuwapa haki zao za kimsingi.

### 3.1.5. Mradi wa uzalishaji bora wa mazao na hifadhi ya ardhi

Uzalishaji duni uliokuwa ukisababisha kipato na lishe duni ni tatizo lililojitokeza wazi na wakulima walilipa kipaumbele swala hili ili lipatiwe ufumbuzi mapema. Katika kutatua tatizo hilo mafunzo mbali mbali ya mbinu bora za kuzalisha mazao ya kilimo na kuhifadhi ardhi yametumika kupunguza ama kuondoa tatizo hili. Hamasa kuu ilikuwa ni kuimarisha uzalishaji na kuhakikisha mfumo dume unafutika kuanzia ngazi ya kaya. Wanawake na wanaume wameelimishwa na kuona faida zinazopatikana kama kaya nzima ikijihusisha na uzalishaji na vilevile kupanga pamoja matumizi ya mapato yanayopatikana baada ya kuzalisha.

## 3.2. Mradi wa mafunzo ya uundaji na uongozi wa vikundi vya wakulima

Mradi huu ulianzishwa ili wakulima waweze kudhibiti maliasili zao na kudhibiti njia za uuzaji wa mazao yao (Masoko), kujadili na kupendekeza sera za kushawishi kurekebishwa au na kutengenezwa sera za taifa zinazohusu maendeleo ya wakulima, kuthaminiwa na kutambuliwa jinsi walivyo, kuelewa na kutengeneza dhana ya jinsia na maendeleo, ili kupunguza tofauti za jinsia katika jamii zao na kuchukua hatua za kuzuia kuenea virusi na ugonjwa wa ukimwi ni muhimu wakulima hao kuanzisha vikundi vya wakulima, mtandao na hatimaye kuwa na jumuia.

Mafunzo ya vikundi vya wakulima husaidia kufikia malengo makuu yafuatayo:

- Njia ya kuifikia jamii
- Kusambaza matokeo ya mafunzo haraka
- Kutambua na kugundua ujuzi wa aina mbali mbali
- Wakulima wabunifu na wenye ujuzi maalum hutumiwa kama viongozi au waelimishaji
- Changamoto mbali mbali hubainishwa kupitia vikundi vya wakulima
- Ni njia ya kuweka mawasiliano rahisi baina ya wakulima
- Ni njia ya kuwapa nguvu na sauti wakulima ili wasikike katika ngazi mbali mbali

Ni muhimu vikundi kupewa mafunzo yafuatayo:

- Mafunzo ya uongozi
- Jinsi ya kuainisha malengo ya muda mfupi na mrefu
- Jinsi ya kuratibu shughuli za vikundi
- Jinsi ya kuweka kanuni za vikundi
- Jinsi ya kuunganisha vikundi mbali mbali
- Jinsi ya kuunganisha wakulima na kuwa na jumuia (Association)
- Kujenga uwezo wa kubaini na kutetea haki za wakulima
- Jinsi ya kutengeneza bajeti ya miradi mbalimbali binafsi na katika vikundi

Mafanikio ya vikundi yatakuwepo kupitia haya yafuatayo:

- Hiari ya watu kujiunga na kikundi
- Dhamira ya kujituma kati ya wanakikundi
- Uongozi mzuri na mawasiliano mazuri katika kikundi
- Matumizi mazuri ya kanuni na usimamiaji mzuri wa kanuni hizo
- Kuwepo mgawanyo mzuri wa faida
- Kuwa na malengo machache
- Kuepuka kuwa tegemezi
- Vikundi viazishwe ili kukabili matatizo yaliyopo katika jamii hiyo

### 3.2.1. Jinsi gani wanaweza kuunda na kuanzisha vikundi

Ili kikundi kiazishwe na kiwe endelevu ni lazima mambo muhimu yafuatayo yawepo:

- Watu
- Mahusiano mazuri kati yao
- Hiari ya watu hao kuanzisha kikundi
- Wazo la kuazisha kikundi lazima lianzie kwao
- Kikundi kianzishwe ili kutatua tatizo linaloathiri jamii hiyo ambalo ndilo litakuwa lengo kuu la kikundi
- Lazima kuwepo na kanuni au katiba itakayokuwa dira ya kikundi
- Ili kurahisisha usimamizi na utekelezaji ni lazima kikundi kiwe na mpango wa kazi
- Ushirikishwaji wa kila mwana kikundi kuazia matayarisho hadi utekelezaji ni muhimu sana
- Usimamizi wa kikundi lazima uwe chini ya kamati ya utekelezaji

## 3.3. Uendeshaji wa shughuli za vikundi

### 3.3.1. Kikundi cha wakulima Matumbulu

Katika kijiji cha Matumbulu, Kata ya Mpunguzi kuna kikundi kiitwacho "Atomic Speed Group" kilichoanzishwa mnamo mwaka 1992. Bwana Peter Wilson mkulima mbunifu na katibu wa kikundi alieleza kuwa shughuli za kikundi zimegawanyika katika sehemu kuu mbili, shughuli za kikundi (za pamoja) na shughuli za mtu mmoja mmoja.

Lipo shamba la kikundi ambalo wanakikundi hutumia kwa kuzalisha nyanya pamoja na mboga mboga za aina mbalimbali. Shamba hilo hupata maji ya kumwagilia kutoka kwenye bwawa la kijiji. Ili kurahisisha usimamizi wa kazi kila mwanachama amegawiwa eneo

lake katika shamba hilo. Wanakikundi hununua kwa pamoja pembejeo kama vile mbolea na madawa na kuelimishana jinsi ya kuzitumia. Vyanzo vya mapato ya kikundi ni ada pamoja na michango itokanayo na mapato. Kiwango cha uzalishaji na aina za mboga mboga au nyanya hutegemea zaidi mahitaji ya soko. Mapato yatokanayo na uzalishaji katika shamba la kikundi hutumiwa na wanakikundi kuendesha shughuli zao binafsi kama vile;kilimo cha mboga mboga katika mashamba yao binafsi, kilimo cha zabibu, usagaji wa nafaka na ufugaji wa samaki. Baadhi ya wanakikundi wamefanikiwa katika hatua mbalimbali:


- Kujenga nyumba bora
- Kununua mashine za kusaga nafaka
- Kupanua mashamba yao binafsi
- Kununua mifugo
- Kununua magari
- Kuwa na mitaji ya kufanyia biashara nyingine.



*Picha shamba la kikundi*

Aidha, zipo shughuli za mtu mmoja mmoja kama vile uvunaji wa maji ya mvua, ufugaji wa samaki, usagaji wa nafaka, kilimo cha zabibu na kilimo cha umwagiliaji. Mkulima mbunifu Bwana Peter Wilson alionesha mashine aliyobuni ili kupunguza mzigo wa kumenya karanga. Mashine hiyo ina uwezo wa kumenya magunia 12 ya karanga kwa saa moja badala ya mtu mmoja kumenya debe moja kwa siku tatu. Vile vile anayo chekeche inayoweza

kuchambua gunia mbili kwa nusu saa badala ya mtu mmoja kuchambua debe moja la karanga kwa siku 2. Mkulima huyu aliweza vile vile kugeuza korongo kuwa bwawa la samaki. Katika shughuli zake za umwagiliaji ameweza kubuni mbinu ya kutumia maji kidogo kwa kutumia debe moja la maji kumwagilia mche mmoja wa nyanya tangia kupanda hadi kuvuna. Ili kuonesha umuhimu wa kutumia rasilimali alizonazo washiriki wa ziara walishangaa walipoona Bwana Peter anatumia maganda ya karanga kama matandazo na kusaidia kuhifadhi unyevu wa udongo. Wakulima walisisimka kwa jinsi mkulima huyu alivyoweza kutumia rasilimali alizonazo kujiendeleza.



*Mashine ya kumenya na kuchambua karanga. Imetengenezwa na Bwana Wilson*

### 3.3.2. Kikundi cha wakulima Chitego

Katika kijiji cha Chitego, Tarafa ya Zoisa, Wilaya ya Kongwa kuna shamba la kuzalisha mbegu ya mahindi linalomilikiwa na wakulima wawili: Bwana Jairos na Bwana Mathias. Wakulima hawa ni kati ya wanakikundi wa kikundi kiitwacho ZOSEMU. Kutokana na shughuli za kikundi hiki wanaziara walijifunza mambo muhimu yafuatayo:

#### 3.3.2.1. Kanuni za uzalishaji mbegu za mahindi

(i) Kabla ya kutayarisha shamba hakikisha shamba lako lipo umbali wa mita 200 au zaidi toka mashamba mengine. Hii husaidia kuondoa tatizo la mwingiliano wa mbegu zisizotakiwa kupitia chavua zinazosafirishwa na upepo.

(ii) Hakikisha mbegu za msingi unazinunua toka mashamba ya serikali

(iii) Tumia nafasi ya kupandia inayoshauriwa na wataalam (Kwa mfano mbegu aina ya Staha-hupandwa sentimita 75 mstari hadi mstari na sentimita 30 mmea hadi mmea)

(iv) Tumia mbolea aina ya fosforasi wakati wa kupanda na weka mfuto wa kifuniko cha soda kwa kila shimo la kupandia.

(v) Baada ya palizi la kwanza tumia mbolea ya kukuzia kama vile (Urea na Sulphate of ammonia) kwa kuweka mfuto wa kifuniko cha soda kwa kila shina (5 g)

**Angalizo**
*Kama mbolea ya samadi inapatikana basi ni vema kuitumia wakati wa kupanda*

### 3.3.2.2. Jinsi ya kuvuna mbegu za mahindi

(i) Baada ya mahindi kukomaa na kukauka vizuri anza kuyavuna

(ii) Ukishayatoa shambani toa maganda ya juu na kisha kata robo ya kwanza na ya mwisho na pukuchua nusu ya kati kwa ajili ya kutayarisha mbegu

(iii) Robo mbili zitumiwe kwa matumizi mengine na si kwa mbegu

### 3.3.2.3. Jinsi ya kukausha mbegu ya mahindi

(i) Jenga chanja yenye kimo kisichopungua mita 1 kwa ajili ya kukaushia mahindi

(ii) Mahindi yaliyokauka vizuri huwa na unyevu usiozidi asilimia 13 na uotaji wake usipungue asilimia 85.

(iii) Kama hakuna kipimo halisi cha kupimia unyevu basi tumia meno yako kwa kuuma hindi na kama ukiuma likapasuka haraka na ukaona linatoa unga unga basi amini kuwa mahindi hayo yamekauka vizuri

**Angalizo**

*Kwa kawaida shamba likitunzwa vizuri hutoa kati ya gunia 20 hadi 28 za kilo 100*

*(i) Hakikisha unaondoa mbegu za magugu kwenye mahindi*

*(ii) Baaada ya kukausha mbegu ziwekwe dawa tayari kwa kuuza*

Kikundi cha uzalishaji mbegu za mahindi kina matatizo makuu mawili

- Hali mbaya ya hewa (Ukame)
- Ushindani wa soko na mashirika makubwa

## 3.4. Benki mazao

Katika kijiji cha Chitego, Tarafa ya Zoisa, Wilaya ya Kongwa na katika kijiji cha Ikowa, Tarafa ya Chilonwa, Wilaya ya Dodoma Vijijini wanaziara walinufaika sana kukutana na vikundi vinavyoendesha Benki mazao. Vikundi hivi vilianzishwa na wanavijiji wachache ili kukabiliana na matatizo yafuatayo:

- Upungufu wa chakula katika kaya hasa katika kipindi cha kulima
- Ukosefu wa mbegu bora za kupanda
- Bei ndogo ya mazao
- Ukame

### 3.4.1. Utekelezaji (Kukabiliana na matatizo yaliyotajwa)

Baada ya njaa iliyokumba eneo lao mwaka 1998 ambayo ilipewa jina *"Ng'airo"* wanavikundi waliamua kutumia nguvu zao kuanza kujenga maghala ya kuhifadhia mazao. Shirika la Kimataifa la Kujitolea la Walei la Italia (LVIA) lilitoa msaada wa fedha taslimu shilingi (TSh) laki tano kwa kila kikundi baada ya kuona juhudi zao na hivyo kuwasaidia kujenga na kumaliza majengo haraka.

### 3.4.2. Namna benki mazao zinavyofanya kazi

- Wanachama pamoja na wanakijiji hutunza akiba ya chakula ambayo huitwa akiba ya kawaida. Lengo la akiba hii ni kuwawezesha wanakijiji kupata hifadhi bora ya chakula na kila mtu anaweza kuweka kwa kiwango anachotaka. Akiba nyingine ni akiba ya mbegu na akiba ya kumudu soko ambayo humsaidia mkulima kuuza mazao kwa bei nzuri. Kwa mfano mkulima akiuza mahindi benki mazao hupata bei ya wakati wa mavuno baada ya muda bei hupanda na

benki mazao huuza mahindi hayo na wakulima hulipwa malipo ya pili

- Wanazo hisa za wanachama na hisa moja ni gunia moja la debe sita
- Kuhakiki uhakika wa chakula kwa kila kaya. Hifadhi ya chakula hugawiwa katika awamu tatu. Awamu ya kwanza ni wakati wa kulima, ya pili wakati wa palizi ya kwanza na ya tatu wakati wa palizi ya pili. Kama mtu akimaliza akiba yake ya chakula anaruhusiwa kukopa na wakati wa kurudisha hulipa asilimia 50 ya mkopo kama riba. Akichukua akiba yake tu bila nyongeza basi halipi riba.
- Ili kumudu gharama nyinginezo kama vile kununua madawa na kulipa walinzi pamoja na posho, kila mkulima hulipia debe moja kwa debe sita anazohifadhi katika benki
- Benki mazao hutoa mikopo kwa wanachama na wakulima wanaoweka mazao yao kwenye benki tu, na ukipewa mkopo wa gunia moja basi unarudisha magunia mawili.

Benki mazao inayo kamati ya utendaji ambayo kazi zake ni:

- Kuwaeleza wateja ubora wa mahindi yanayotakiwa kuwekwa
- Kudhibiti ubora wa mahindi au mazao yanayopokelewa
- Kuweka mazao ya wakulima kama yatakuwa yamefikia kiwango kinachokubalika
- Kuweka alama (kuandika jina) magunia ya wakulima ambayo hayajafikia kiwango ili wakati wa kuchukua wachukue mazao waliyoleta wenyewe na si vinginevyo.

**Angalizo**:
Vigezo vikuu vya ubora ni mazao yawe yamekaushwa vizuri na yasiwe na wadudu

## 3.5. Chama cha ushirika na mikopo vijijini (CAVi ushirika Ltd)

Kabla ya CAVi kuanzishwa, katika vijiji husika kulikuwa na vikundi vidogo vidogo vya uzalishaji na kugawana mapato na vile vile kukopeshana. Wakati wa kilimo watu walikosa pesa za kununulia pembejeo. Mahitaji ya mikopo yalitegemea sana utaratibu wa kimila uitwao **Songolenda** uliolenga kukopeshana ili kusaidiana katika misimu yenye matatizo kama njaa. Wakati huo kama ulikopa debe la mahindi ulikuwa unarudisha debe tatu hadi sita kitu ambacho kilizidi kuwaneemesha matajiri kwani viwango vya riba vilipanda kutegemea ugumu uliopo. Ili kujikwamua wakulima walijiunga kwenye vikundi vidogo vidogo. Baada ya kuona kwamba upatikanaji wa pesa kupitia vikundi vidogo vidogo ulikuwa mgumu na mikopo ya watu binafsi ilikuwa na riba kubwa ndipo wananchi walipoamua kuunganisha vikundi vyote na kupata kikundi kimoja kikubwa kiitwacho CAVi.

CAVi ni chama cha Akiba na Mikopo kilichoundwa na wakazi wa kata ya Zoisa. Chama hiki kinajumuisha wanachama kutoka katika vijiji vya Mlanje, Matongoro, Nolini, Makawa na Mkoka. Mnamo mwaka 1995, LVIA iliipa kazi INADES ya kufanya utafiti wa mahitaji ya kilimo katika Tarafa ya Zoissa. Matokeo ya utafiti yalionesha kuwepo kwa uwezo mkubwa wa kiuchumi na kijamii. Uwezo huo ulikuwa ni:

- Uzalishaji mkubwa wa mahindi
- Shughuli za kiuchumi na biashara
- Utaratibu wa kuweka na kukopa ulio katika mila za wenyeji
- Kuwepo kwa mahitaji ya mikopo
- Kuwepo kwa vikundi vya wakulima kama chanzo cha kufanyia shughuli za akiba na mikopo
- Kuwepo kwa sheria zinazoruhusu uanzishwaji wa vyombo vya akiba na mikopo

Mnamo mwaka 1997 INADES iliwaunganisha wanakikundi na kuunda kamati zifuatazo:

- Kamati ya katiba
- Kamati ya ujenzi
- Kamati ya fedha na mikopo

INADES ikishirikiana na LVIA waliendesha mafunzo mbali mbali kama vile jinsi ya kuanzisha vyama vya kuweka na kukopa na kuwezesha kufanyika ziara za mafunzo. Mnamo mwaka 1998 wanachama waanzilishi walikuwa 115, ambao waliamua kutumia nguvu zao na kuanza kujenga ghala. Jumla ya michango toka kwa wanachama ilikuwa ni shilingi 1,500,000/=. LVIA walipoona tayari wanachama wamechanga kiwango cha pesa kilichotajwa basi nao waliamua kuwaongezea kiwango sawa na walichochanga hivyo zikapatikana jumla ya shilingi 3,000,000.

Mnamo mwaka 2000 chama kilisajiliwa kikiwa na malengo makuu yafuatayo:

- Kuinua hali ya maisha ya wanachama
- Kutoa mikopo nafuu kwa wakulima
- Kutoa mikopo ya pembejeo kwa wakulima
- Kuhamasisha wakulima kuhusu kuweka na kukopa
- Kutoa elimu ya ushirika kwa wanachama

Uendeshaji

- Wanachama wanazo amana za kawaida ambazo hazina riba
- Ipo amana ya mkataba ambayo mwanachama au mteja huweka fedha kwa kipindi maalum kama vile miezi 3, 6 au 12

## 3.5.1. Aina za mikopo zitolewazo na ushirika

- Mkopo wa kilimo
- Mkopo wa biashara
- Mkopo wa dharura
- Mkopo wa elimu

### 3.5.2. Sera ya utoaji mikopo iko kama ifuatavyo

Kilimo

- Mwanachama hukopa mara mbili ya hisa zake
- Marejesho ni baada ya miezi minane
- Riba ni asilimia tatu (3%)
- Mkopo hutolewa mwezi Novemba na Desemba

Biashara

- Mwanachama anakopa mara tatu ya hisa alizonazo
- Mwanachama anakaa na mkopo kwa miezi minne
- Marejesho ni kwa awamu nne
- Riba ni asilimia tano (5%) kwa kila mwezi

Jamii

- Hutolewa wakati wowote kwa mwanachama
- Kiwango cha mkopo ni asilimia thelathini (30%) ya hisa za mwanachama
- Marejesho huchukua miezi mitatu kwa riba ya asilimia nane (8%) kwa mwezi

Vifaa

- Mkopo wa vifaa/zana za kilimo
- Mkopaji analipia nusu ya mkopo
- CAVi inadhamini nusu ya mkopo
- Marejesho ya mkopo ni baada ya mwaka mmoja
- Riba asilimia tatu (3%)

### 3.5.3 Hali ya chama kwa sasa

- Mwaka 1999 walianza na mkopo wa shilingi 1,000,000/= na sasa wamekopesha shilingi 102,000,000/=
- Wanachama wameongezeka toka 115 hadi 280 na kati yao wanaume ni 165 na wanawake 105.
- Jumla ya wateja na wanachama ni 429

- Hisa za kawaida ni shilingi 14,971,280/=
- Amana za kawaida ni shilingi 4,649,805/=
- Amana maalum ni shilingi 7,811,945/=

Chama hiki kina uhusiano wa karibu na MVIWATA, INADES, LVIA, Chuo cha Ushirika Moshi na Serikali ya Kijiji.

## 3.6. Hifadhi ya mazingira na matumizi bora ya udongo

Katika kijiji cha Chamkoroma Wilaya ya Kongwa yapo mambo mengi yanayofanywa na kamati ya mazingira. Kamati hii ilianzishwa mwaka 1995 kwa kushirikiana na wakufunzi toka INADES. Kamati inaundwa na wajumbe 12 kutoka katika vitongoji 6 vya kijiji.

### 3.6.1. Shughuli za kamati

- Kuhamasisha jamii na kusimamia shughuli zote za hifadhi ya mazingira
- Kuhamasisha kilimo endelevu
- Kuhamasisha na kusimamia vikundi vya upandaji wa miti
- Kusaidiana na wataalam kuelimisha wanakijiji juu ya umuhimu wa kuhifadhi mazingira
- Kusimamia sheria ndogo ndogo walizojiwekea wanakijiji ili kuhifadhi mazingira

### 3.6.2. Sheria zinazotumiwa na kamati ya mazingira

(i) Ni marufuku kuchoma misitu ovyo
(ii) Ni marufuku kulima ovyo katika sehemu za milimani

Mtu yeyote anayevunja sheria hizi hulipa faini ya shilingi 5,000/= (Kasunzu) au hushitakiwa na kuhukumiwa kifungo cha miezi 6.

Kamati imekuwa ikiendesha na kusimamia vikundi vidogo vi vinavyoshughulika na hifadhi ya mazingira kwa kufanya shu mbali mbali zifuatazo:-

- **Hifadhi na matumizi bora ya ardhi** kama vile kilimo makinga maji na upandaji wa miti ya mbao na matu katika sehemu za milimani. Katika eneo hili mbinu m mbali zinatumika kuziba makorongo yaliyosababishwa mmomonyoko wa udongo na vile vile upandaji wa unafanywa kuzuia mmomonyoko kwenye kingo za mito. kipo kilimo cha umwagiliaji cha mboga mboga na matu kwa kutumia maji ya mvua yaliyovunwa na maji yaliyote kutoka vyanzo vya maji vinavyohifadhiwa milimani.

- **Matumizi ya biogesi, majiko banifu na ufugaji wa san** ni miradi mbadala inayofanyika kijijini ili kupunguza uhar wa mazingira kama vile ukataji miti kwa ajili ya nishat kuchoma mkaa kama chanzo cha pato katika kaya

- **Ufugaji wa mbuzi wa maziwa na kilimo cha mb mboga** husaidia kuboresha lishe za wanakijiji na vile kuinua pato la kaya.

> **Angalizo**:
> Vikundi hivi huundwa na watu wachach walioshibana kama vile marafiki, kaya moja a muunganiko wa zaidi ya kaya moja.

## 3.6.3. Mafanikio

- Kwa mwaka jana peke yake kijiji kimepanda jumla ya mi matunda na mbao 247,078
- Kijiji kimeweza kuandaa mpango wa kazi pamoja masomo kwa kusaidiwa na INADES
- Kijiji hiki ni mwanachama wa Muungano wa Vikundi Wakulima Tanzania (MVIWATA), Taifa

- Kamati ya mazingira imesaidia sana katika kusuluhisha migogoro mbali mbali katika kijiji kwa kushirikiana na serikali ya kijiji
- Wanakijiji pamoja na wanakamati wamepata fursa za kuhudhuria warsha na semina mbali mbali za mafunzo
- Familia ya Katibu wa mazingira Bwana Rafael Chinolo pamoja na mkewe Bi Jesca Chinolo mwaka huu wamepanda jumla ya miti 6,161. Hii inafanya jumla ya miti ya mbao na matunda waliyonayo kuwa 16,161.

## 3.7. Ujuzi asili

Katika vijiji vya Chamkoroma na Mkoka kuna vikundi vya matibabu ya asili. Wanavikundi kwa umahiri mkubwa walieleza jinsi wanavyoweza kutumia elimu ya mababu zao kukabiliana na matatizo yafuatayo:

- Matatizo ya mimea shambani
- Hifadhi ya nafaka baada ya mavuno
- Magonjwa ya mifugo
- Hifadhi ya mbegu
- Magonjwa ya watoto na akina mama
- Magonjwa ya akina baba

Wanaziara walipata maelezo ya kina kuhusu dawa zifuatazo:

### 3.7.1. Dawa ya kuzuia panya wanaofukua mbegu zilizopandwa shambani

Kutatua tatizo hili mbegu za mti wa Mzege zege hutumika kama ifuatavyo:

(i) Ponda mbegu zake hadi upate unga laini
(ii) Changanya unga ulioupata na maji kiasi
(iii) Weka mbegu zako kwenye chombo kama beseni

(iv) Changanya vizuri mbegu na unga uliopo kwenye maji
(v) Hakikisha kila mbegu imepata dawa vizuri
(vi) Panda mbegu siku hiyo hiyo baada ya kuziwekea daw.

### 3.7.2. Dawa ya kuzuia sondo (Stalk borer) kwenye mahindi shambani

(i) Chukua mchanga kutoka shambani mwako
(ii) Jaza kiasi mchanga huo kwenye tumba la mhindi
(iii) Baada ya hapo sondo hufa

### 3.7.3. Dawa ya kuhifadhi nafaka

(i) Chukua majani ya mwarobaini na kuyatwanga
(ii) Loweka magunia kwenye maji yaliyochanganywa na majani ya mwarobaini (yaliyotwangwa) kwa muda wa saa 12
(iii) Toa magunia na yaanike kwenye kivuli mpaka yakauke
(iv) Yakisha kauka yatumie kuhifadhia nafaka

### 3.7.4. Kuhifadhi maharage kwa kutumia vumbi la ulezi

(i) Vuna ulezi na kuukausha vizuri
(ii) Peta ulezi ili kupata vumbi lake
(iii) Changanya vizuri vumbi la ulezi na maharage na kisha hifadhi maharage hayo kwenye gunia au kiroba

### 3.7.5. Kuhifadhi mahindi

(i) Vuna mahindi toka shambani
(ii) Pukuchua mahindi na kuyaanika ili yakauke vizuri
(iii) Kusanya mahindi na vumbi lake

(iv) Changanya majivu ya taka taka za maharage na majivu ya magunzi

(v) Majivu ya kinyesi cha ng'ombe changanya na jivu la pumba za mpunga

(vi) Michanganyiko yote hiyo ichanganywe na mahindi na vumbi lake na kuhifadhiwa

## 3.7.6. Dawa ya ukungu na wadudu kwenye bustani za mboga mboga

Kutumia majani ya mwarobaini:

(i) Twanga lita moja au kilo moja ya majani ya mwarobaini

(ii) Weka robo kipande cha sabuni ya kufulia

(iii) Chukua lita 20 za maji ongeza lita 1 ya mwarobaini halafu kwenye mchanganyiko huo ongeza gramu 20 za pilipili kichaa

(iv) Acha mchanganyiko huo kwa muda wa saa 24

(v) Baada ya hapo chuja mchanganyiko huo

(vi) Dawa hiyo ipigwe mara 2 katika muda wa siku saba.

Kutumia minyaa na utupa

(i) Chukua matone ya utomvu wa minyaa changanya na kilo 4 ya utupa

(ii) Ongeza maji lita 15 na kisha ongeza lita moja ya bangi ya mbwa

(iii) Kwenye mchanganyiko ulio hapo juu ongeza mashona nguo (*Bidens pilosa)* kilo moja na omo kilomoja na acha mchanganyiko huo kwa saa 12 kisha chuja na dawa itakuwa tayari kwa matumizi

## 3.7.7. Dawa za mifugo

### 3.7.7.1. Jinsi ya kutibu minyoo ya ng'ombe na mbuzi

(i) Chukua shubiri mwitu (*Aloe*) itwange halafu kamua utomvu wake

(ii) Chukua utete au mwanzi wenye ukubwa sawa kidole gumba cha mkono
(iii) Chukua utomvu wa shubiri mwitu jaza kwenye ut na ukaushe
(iv) Ukisha kauka kata vidonge vyenye urefu sentimita 2.5
(v) Chukua kilo 4 za pumba changanya na maji lita weka kidonge kimoja koroga vizuri mpa mchanganyiko ulainike
(vi) Gawanya mchanganyiko huo mara saba
(vii) Mpe mnyama kila siku kwa muda wa siku saba

**3.7.7.2. Kinga au tiba ya minyoo ya ng'ombe na mbuz (Mhumo au Mdachi)**

(i) Chukua majani 3 na maganda 3 kutoka kwenye mt wa mhumo
(ii) Maganda na majani hayo yachanganywe na lita 2 za maji
(iii) Mchanganyiko huo uchemshwe hadi maji yabadilike rangi na kati ya lita 2 ibakie kama lita 1.5
(iv) Kwa mbuzi apewe chupa ya soda ya mchemsho huo
(v) Kwa ng'ombe apewe lita 1 ya mchemsho huo

# 4. Mafunzo mengine

Washiriki wa ziara waliweza kujifunza mambo mengine muhimu ambayo yalitokana na maswali yaliyoulizwa siku ya majumuisho ya ziara kama vile:-

- Uzalishaji na ufugaji wa kuku wa kienyeji
- Magonjwa muhimu yanayoshambulia kuku wa kienyeji pamoja na dalili zake
- Kinga/chanjo pamoja na madawa yanayotibu magonjwa hayo ya kuku wa kienyeji

- Kutumia raslimali zinazokuzunguka ili kubuni miradi itakayo leta kipato katika kaya au kuhifadhi mazingira kwa ujumla

Katika majadiliano wanaziara waliweza kubadilishana uzoefu katika kutumia tiba asilia kwa mifugo na binadamu na pia matumizi ya dawa asili za kuhifadhi mazao baada ya mavuno. Pia swala la Ukimwi lilijitokeza sana kwa wanaziara kukubaliana kwamba tatizo la ukimwi ni kubwa. Hivyo makubaliano yalikuwa kwamba kila mwanaziara apeleke ujumbe huko aliko pamoja na wanaziara wenyewe kuwa mfano hai katika kupambana na ukimwi.

## 5. Hitimisho

Katika ziara zote mbili washiriki waliwapongeza sana wakulima na wafugaji wabunifu waliowatembelea. Katika majadiliano kila mwanaziara alisema alikuwa anastaajabu mambo waliyokuwa wanayaona kila walikotembelea na wengi walikuwa na ari kwamba wakirudi sehemu zao wangejitahidi kufanya jambo ambalo kila mmoja alilifurahia kipekee. Kwa mfano ufugaji wa samaki, kupanda miti ya mbao katika sehemu zenye mmomonyoko wa ardhi, kuzalisha gesi kwa kinyesi cha ng'ombe na kutumia makorongo kuhifadhia maji ya mvua kwa matumizi ya umwagiliaji.

Wanaziara walihamasishana kwamba waache uvivu na wawe mstari wa mbele katika ubunifu mbalimbali ili wawe chachu kwa wengine. Pia mwanaziara mmoja aliwaasa wenzake kwamba kwa chochote walichoahidi kukifanya baada ya ziara hii, ni kwamba kweli watafiti wa mradi watawatembelea na kuona kama ahadi zilizotolewa zimetekelezwa. Kwa hiyo wasibweteke ili wasije wakapata aibu.

Ni imani yetu kwamba washiriki wa ziara watafaidika na waliyoyaona na pia ni matarajio kwamba kila mwanaziara anaweza akabuni shughuli fulani ya kumletea maendeleo yeye mwenyewe au kwa ujumla jumuia anayoishi.

## 6. Tathmini ya ziara ya mafunzo INADES

- Wanaziara wengi wamefurahishwa na maandalizi ya ziara kwa ujumla
- Wengi wamevutiwa sana na benki mazao inavyofanya kazi na kusaidia kuinua kipato cha wanavijiji na hasa kuimarisha uhakika wa chakula kwa kaya
- Wanaziara wamefurahishwa sana kubadilishana uzoefu wao kwa wao
- Wakulima wengi wametoa ushauri kwamba ziara kama hizi ziwepo kwa wingi ili kuleta mabadiliko ya haraka katika jamii yetu na taifa kwa ujumla wake
- Uendeshaji wa kazi za vikundi na pia mtu mmoja mmoja imewafurahisha wakulima wengi
- Wakulima wengi wamefurahishwa na jinsi wawezeshaji wanavyoweza kuibua changamoto kwa kupitia mchakato kati yao na wakulima
- Baadhi ya wakulima wamelalamikia muda wa ziara kuwa mfupi na kusema kuwa ndiyo maana muda wa mjadala unafupishwa ili tuweze kumaliza mambo yote yaliyopangwa kufanyika wakati wa ziara
- Wakulima wengi wameshauri kuongeza idadi ya washiriki ili elimu ienee kwa watu wengi kwa wakati mfupi
- Kamati ya mazingira imetoa mfano mzuri kwa washiriki wengi kwa sababu ya kuwa na mpango kazi mzuri kwa faida ya wanakijiji wake

### 6.1. Tathmini ya wakufunzi wa INADES walioshiriki

- Wanaziara walikuwa huru kuchangia hoja zao na vile vile walinunua vitabu kwa wingi ili waelimike zaidi
- Maandalizi yalikuwa mazuri na vitendea kazi vilikuwa vya kutosha

- Wakulima walionesha uelewa mkubwa jinsi ya kumudu mazingira yao na walionesha kiu kubwa ya kujifunza mambo mapya
- Timu ya TARP II-SUA ilikuwa makini sana na kuuliza maswali ya uchokozi ambayo yalisaidia sana wanaziara kuelewa vizuri zaidi mada mbali mbali

## 6.2. Maoni

- Wanaziara hawakupata muda wa kutosha kuuliza maswali yao
- Waandaaji hawakupeleka habari kwa wakulima wao kuwaeleza kama kuna ugeni ndiyo maana muda mwingi ulipotea tulipotembelea kijiji cha Mkoja
- Wanaziara wengi hawakujua lengo la ziara kabla ya ziara
- Baadhi ya wakulima walionesha kutaka kutawala majadiliano na hivyo kuwanyima nafasi wachangiaji wapya

# 7. Viambatanisho

## 7.1 Washiriki ziara ya kwanza

| | Jina | Jinsia | Kazi | Kijiji | Kata | Wilaya | Anwani |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Edward F. Nziku | Me | Mkulima | Kisilo | Uwemba | Njombe | S.L.P. 54 Njombe |
| 2 | Hassan M. Jumadari | Me | Mkulima | Kabukunda | Mgambo | Handeni | S.L.P. 44 Handeni |
| 3 | Simon P. Myogo | Me | Mkulima | Kidudwe | Mtibwa | Mvomero | S.L.P. 55 Morogoro |
| 4 | Zakaria M. Saidi | Me | Mkulima | Mponela | Isandula | Mbozi | S.L.P. 303 Mbozi |
| 5 | Hawa H. Mgonja | Ke | Mkulima | Lungo | Mtibwa | Mvomero | S.L.P. 16 Mvomero |
| 6 | Douglas M. Kiwango | Me | Mkulima | Simike | Utengule Usangu | Mbarali | S.L.P. 64 Mbarali |
| 7 | Eneles Eliakimu | Ke | Mkulima | Matebete | Chimala | Mbarali | S.L.P. 123 Mbarali |
| 8 | Sabela Kayuni | Ke | Mkulima | Mpondela | Isandula | Mbozi | S.L.P. 303 Mbozi |
| 9 | Mwanaisha Sango | Ke | Mkulima | Jaira | Madanga | Pangani | S.L.P. Madanga Pangani |
| 10 | Paschary P. Mgaya | Me | Mkulima | Utelewe | Igosi | Njombe | S.L.P. 253 Njombe |
| 11 | Christina Simon (Mwinga) | Ke | Mkulima | Kidudwe | Mtibwa | Mvomero | S.L.P.55 Mvomero |
| 12 | Wahabi Bakari | Ke | Mkulima | Azimio Mswiswi | Igurusi | Mbarali | S.L.P. 336 Mbarali |
| 13 | Mathayo J. Tillya | Me | Mkulima | Mkata | Mkata | Handeni | S.L.P. 164 Handeni |
| 14 | Kiroka R. R. S. | ? | Mkulima | Madanga | Madanga | Pangani | S.L.P. 58 Pangani |
| 15 | Juma H. Mwampiki | Me | MKulima | Simiwe | Utengule Usangu | Mbarali | S.L.P. 64 Igurusi Mbarali |
| 16 | Anamaria B. Komba | Ke | Mkulima | Mtama | Utiri | Mbinga | S.L.P. 28 Mbinga |
| 17 | Victor S. Luvinga | Me | Mkulima | Uwemba | Uwemba | Njombe | S.L.P. 439 Njombe |
| 18 | Leonard D. Msongole | Me | Mkulima | Ivwanga | Mlowo | Mbozi | S.L.P. 277 Mbozi |
| 19 | Sophia O Kaney | Ke | Mkulima | Matebete | Chimala | Mbarali | S.L.P. 123 Mbarali |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 20 | Kudra S. Msumi | ? | Mkulima | Mkuranga | Mkuranga | Pwani | S.L.P. 10 Mkuranga, Pwani |
| 21 | Jostina S. Ngulo | Ke | Mkulima | Igodivaha | Imalinyi | Njombe | S.L.P. 34 Njombe |
| 22 | Rukia Njau | Ke | Mkulima | Lungo | Mtibwa | Mvomero | S.L.P. 16 Mvomero |
| 23 | Beatrice M. Ntauka | Ke | Afisa Ughani | MODECO B | Mbuyuni | | Morogoro |
| 24 | Antoneta Kayombo | Ke | Mkulima | Falkland | Mbuyuni | Morogoro | S.L.P. 3000 Morogoro |
| 25 | Salehe K. Mdengo | Me | Mkulima | Mtamba | Mbuyuni | Morogoro | S.L.P. 610 Morogoro |

## 7.2 Washiriki wa ziara ya pili

| | Jina | Jinsia | Kijiji | Wilaya | Anwani |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Elizabeth Kajiba | Ke | Kikusya | Kyela | C/o Shule ya Msingi, S.L.P. 150, Kyela -Mbeya |
| 2. | Amina Mrisho | Ke | Hembeti | Morogoro | C/o Shule ya Msingi Hembeti, S.L.P. 71, Morogoro |
| 3. | Michael M. Mwamafupa | Me | Kikusya | Kyela | Assemblies of God, Busale, S.L.P. 89, Kyela-Mbeya |
| 4. | Fatuma Omari | Ke | Kongo | Bagamoyo | Shule ya Msingi Kongo, S.L.P. 94, Bagamoyo |
| 5. | Bakari S. Salumu | Me | Hembeti | Mvomero | C/o Shule ya Msingi Hembeti, S.L.P. 71, Morogoro |
| 6. | Helena Siwale | Ke | Itepula | Mbozi | S.L.P.125, Mbozi |
| 7. | Eleuter Magovela | Me | Kalenga | Iringa | C/o Shule ya Msingi Kalenga, S.L.P. 225, Iringa |
| 8. | Benito Mwanamhavi | Me | Azimio Mswiswi | Igurusi | S,L.P. 659, Igurusi, Mbeya |
| 9. | Dodo Ole Chabala | Me | Wami Sokoine | Mvomero | S.L.P. 894, Mvomero, Morogoro |
| 10. | Zamzam Iddi Saburi | Ke | Kalenga | Iringa | C/o Shule ya Msingi Kalenga, S.L.P.225, Iringa |
| 11. | Ismail Ole | Me | Matebete | Chimala | Box 39 Chimala - |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Komba | | juu ya benki mazao<br>2. Nitahamasisha wenzangu kuendeleza kilmo cha nyanya na mahindi |
| 17. | Victor S. Luvinga | Ughani | 1. Nitakwenda kuelimisha/kuhamasisha wakulima wa kikundi cha wanyamakazi wawe na benki mazao yao<br>2. Kuandaa mpango wa kazi ambao utahusisha wakulima wa vijiji jirani wawe na benki mazao |
| 18. | Leonard D. Msongole | Mkulima | 1. Nitaenda kufungua Benki mazao<br>2. Kilimo cha nyanya kutumia samadi |
| 19. | Sophia O Kaney | Mkulima | 1. Nitafuga ufugaji wa kisasa kutumia ng'ombe wa kienyeji<br>2. Nitalima karanga kutumia samadi ya asili |
| 20. | Kudra S. Msumi | Mkulima | 1. Nitakwenda kuwashawishi wanakikundi wenzangu tulime kwa kushirikiana na kuboresha ardhi, kutafuta masoko ya pamoja<br>2. Nitalima kwa mpango ili kuzidisha mazao zaidi kuwaelimisha wenzangu jinsi ya kupata mtaji kwa kupitia kilimo cha kitaalamu |
| 21 | Jostina S. Ngulo | Mkulima | 1. Nitakwenda kuelimisha vikundi ushirikiano<br>2. Kuelimisha mama wajane njia za kutorithiwa |
| 22. | Rukia Njau | Mkulima | 1. Nitakwenda kulima kilimo cha kitaalamu kwa kutumia madawa |
| 23. | Beatrice M. Ntauka | Ughani | 1. Kutoa elimu ya benki mazao kwa maafisa ughani wote kata ya Morogoro mjini (19) na mitaa yangu (13) kwa kuitisha vikao vya wananchi kuhamasisha<br>2. Kurekebisha udongo kwenye mradi wa kutumia mawe na kujaza miti kurudisha kwenye hali ya kilimo |
| 24. | Antoneta Kayombo | Mkulima | 1. Kufungua shamba la nyanya<br>2. Kufungua benki mazao |
| 25. | Salehe K. Mdengo | Mkulima | 1. kuanzia msimu ujao, nitalima kama anavyolima ndugu Mathias wa shamba la kutunza mbegu na kupanda vilevile<br>2. Nitaanza kulima nyanya kwa ubora, kama alivyolima ndugu Hosea na wenzake |

## 7.4 Ahadi za Wakulima Ziara ya Pili

| Na. | Jina | Kazi | Ahadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Elizabeth Kajiba | Mkulima | Kuanzisha kilimo cha bustani na ufugaji wa kuku wa kienyeji na kutoa elimu kwa wakulima wenzangu ifikapo 6.03.2005. |
| 2. | Amina Mrisho | Mkulima | Nitahamasisha kikundi chetu kuanzisha kilimo cha bustani na ufugaji wa kuku wa kienyeji ifikapo 20.10.2005 |
| 3. | Michael M. Mwamafupa | Mkulima | 1. Kuzalisha mbegu za vitunguu<br>2. Kuanzisha kikundi cha hifadhi ya samadi<br>3. Kuanzisha kikundi cha watu 4 cha kulima mbogamboga |
| 4. | Fatuma Omari | Mkulima | 1. Kujenga banda bora la ng'ombe wa maziwa<br>2. Kuanzisha hifadhi bora ya samadi<br>3. Kupanda miti |
| 5. | Bakari S. Salumu | Mkulima | Kuboresha kilimo ifikapo Desemba, 2005 |
| 6. | Helena Siwale | Mkulima | Kuhamasisha wakulima wenzangu kuboresha kilimo |
| 7. | Eleuter Magovela | Mkulima | Nitaunda kikundi cha kilimo cha bondeni |
| 8. | Benito Mwanamhavi | Mkulima | 1. Kufundisha na kuimarisha vikundi vya wakulima<br>2. Nitaanzisha ufugaji wa kuku wa kienyeji |
| 9. | Dodo Ole Chabala | Mkulima | 1. Nitajenga zizi la kisasa<br>2. Ifikapo Desemba 2004 nitakuwa nimeanzisha kikundi cha wafugaji |
| 10. | Zamzam I. Saburi | Mkulima | Nitaunda kikundi cha akina mama 6 ili tuanze kurutubisha ardhi kwa kutumia marejea |
| 11. | Ismail Ole Kurprash | Mkulima | 1. Ifikapo 10.10.2005 nitakuwa nimeanzisha kikundi cha wanawake cha ufugaji wa kuku wa kienyeji |
| 12. | Anthony T Rock | Mkulima | 1. Nitaazisha kilimo cha umwagiliaji<br>2. Nitapanda miti 5,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | 3. Nitaanzisha kitalu cha miti isiyopungua 6,000<br>4. Kuendeleza kilimo cha makinga maji<br>5. Kuimarisha kikundi cha hifadhi mazingira |
| 13. | Esther Dikoko | Mkulima | 1. Nitapanda miti 200<br>2. Nitahamasisha akina mama tujenge majiko banifu 10 ifikapo Juni, 2005 |
| 14. | Issa Kimaro | Ughani | 1. Kuboresha ufugaji wa kuku wa kienyeji ifikapo Juni, 2005<br>2. Kuhamasisha wanakijiji kupanda miti ya kivuli na ya kurutubisha ardhi (Lukina, Mlonge) |
| 15. | Danny L.Nyalusai | Mkulima | 1. Ifikapo 30.07.2004 nitakuwa nimeanzisha bustani ya mboga na matunda<br>2. Nitaanzisha ufugaji wa samaki na kikundi cha wafugaji ifikapo 30.12.2004 |
| 16. | Nuhu Ole Shabala | Mkulima | 1 Kujenga banda la kuhifadhi malisho<br>2. Kuanzisha kikundi cha upandaji wa miti ahadi zote zitakuwa tayari ifikapo 30.3.2005 |
| 17. | Athuman Nyagawa | Mkulima | Kuhamasisha kikundi cha wanyamakazi B kupanda miti 1000 ifikapo Aprili, 05 |
| 18. | Sikudhani Fute | Mkulima | 1. Kuanzisha kikundi cha akina mama cha kutengeneza majiko banifu<br>2. Kuboresha ufugaji wa kuku wa kienyeji ifikapo 2005 |
| 19. | Hamisi Palango | Mkulima | 1 Nitaanzisha kikundi cha mazingira na kufuga kuku wa kienyeji ifikapo Mei, 2005 |
| 20. | Esther Munissi | Mkulima | Nitaboresha kuku wa kienyeji, nitaanzisha kikundi cha kulima bustani hadi 2005 |
| 21 | Salum D. Saidi | Mkulima | Kuanzisha kikundi cha wakulima wa mhogo na ufugaji wa kuku wa kienyeji |
| 22. | Yuster T Chuma | Mkulima | Kujenga banda la nguruwe na kuanzisha kitalu cha miti ifikapo |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | Agosti 2004 |
| 23. | A.T.K. Simwaba | Mkulima | 1. Kuanzisha masomo ya vikundi kupitia INADES<br>2. Kulima nyanya<br>3. Kuhifadhi mbolea ya samadi<br>4. Kufuga kuku wa kienyeji, nguruwe na ng'ombe wa maziwa. Yote haya yatakuwa tayari ifikapo mwaka 2005 |
| 24. | Bibi Shamba Magindu | Ughani | 1. Kuhamasisha ufugaji wa kuku wa kienyeji<br>2. Kuunganisha vijana wa kijiweni na kuanzisha kilimo cha bustani |

Printed by InterPress of Tanzania Limited